JESMA
009

# JARIBIO LA MWISHO K.C.P.E
# DARASA LA NANE 2021

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA**
**KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **11.** Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - I pekee.
    A. kahawa, fedha;
    B. chumvi, chupa
    C. sukari, mvua
    D. mali, chai

    Jibu sahihi ni C

    **1** [A] [B] [C] [D]   **11** [A] [B] ▬ [D]   **21** [A] [B] [C] [D]   **31** [A] [B] [C] [D]   **41** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Tovuti: www.jesmapublishersltd.com** **Barua pepe: jesmapublishers@yahoo.com**

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15**. *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Ni vigumu kwa jamii yoyote kupiga hatua __1__ kuwawekea vijana msingi __2__ wa malezi. Ili kuimarisha afya, yaani __3__, watoto hupewa chanjo ya kuzuia maradhi ya __4__. Njia nyingine ni kuanizisha vyuo vya kiufundi vitakavyowapa __5__ za kujiendeleza. __6__, utoaji wa elimu bila malipo __7__ fursa ya kusomea taaluma mbalimbali pamoja na __8__ vipawa vyao. Jamii __9__ watambua vijana huwa haina matarajio mema ya uongozi wa baadaye.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. minghairi ya | B. licha ya | C. mithili ya | D. fauka ya |
| **2.** | A. nzuri | B. mbora | C. jema | D. thabiti |
| **3.** | A. staha | B. rai | C. ari | D. hulka |
| **4.** | A. malaria, pumu waba | B. kichocho, tauni, kifafa | C. pepopunda, surua kupooza | D. mafua, malaria ukambi |
| **5.** | A. stadi | B. maarifa | C. ujuzi | D. hekima |
| **6.** | A. Ama | B. Lau | C. Ilhali | D. Halikadhalika |
| **7.** | A. inawapa | B. kumewapa | C. umewapa | D. tunawapa |
| **8.** | A. kuyakuza | B. kurikuza | C. kuikuza | D. kuwakuza |
| **9.** | A. wakikosa | B. mkikosa | C. likikosa | D. ikikosa |

Moyo wa Amina ulijaa __10__. Machozi yalijikusanya kwenye macho yake __11__ matone makubwa makubwa na __12__ daftari alilokuwa akiliandikia. Hata hakutanabahi mwalimu __13__ na kusimama mbele yake. Mwalimu akamwita ofisini kumsaili na kumliwaza. Kumbe wavyele wake walikuwa __14__ ya kumwoza! Ndipo mwalimu akamtafutia mhisani wa kuyadhamini masomo yake. Ama kweli __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. machozi | B. simanzi | C. nyemi | D. ukiwa |
| **11.** | A. yakamdondoka | B. yakamchuruzika | C. yakatiririka | D. yakambubujika |
| **12.** | A. kuilowesha | B. kuyalovya | C. kulowekana | D. kulilovya |
| **13.** | A. alivyoingia | B. alioingia | C. alipoingia | D. akaingia |
| **14.** | A. wamekula nyama | B. wamepika majungu | C. wameshika miko | D. wametia mrija |

**15.** A. mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina
B. Mungu akiziba hapa huzibua pale
C. mpanda farasi wawili hupasuka msamba.
D. mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

*Kuanzia nambari* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu lifaalo zaidi.*

**16.** Chagua kauli ya **kutendewa** ya:
Tatu alichukua pete ya zawadi
A. Pete ya Zawadi ilichukuliwa na Tatu.
B. Pete ilichukuliwa Tatu kwa Zawadi.
C. Zawadi alichukuliwa pete na Tatu.
D. Zawadi alichukuliwa pete kwa Tatu.

**17.** Maneno yafuatayo yatafuatana vipi katika kamusi?
*i) mchuuzi*
*ii) mchumba*
*iii) muhogo*
*iv) muhina*

A. (ii), (i), (iv), (iii)
B. (iv), (iii), (ii), (i)
C. (ii), (i), (iii), (iv)
D. (i), (ii), (iv), (iii)

**18.** Chagua sentensi yenye **kwa** inayoonyesha "pamoja na".
A. Seme alipendwa kwa heshima yake.
B. Tulienda moja kwa moja hadi uwanjani.
C. Wake kwa waume walishiriki sherehe hiyo.
D. Nuru alipata alama saba kwa kumi.

**19.** Mtu mwenye ujuzi wa kufua visu ni
A. mjume
B. mjumu
C. mhandisi
D. mhazili

**20.** Chagua kukanusha kwa:
Kocha alikuwa akiwapongeza na kuwahimiza wachezaji.
A. Kocha hakuwa akiwapongeza kwa kuwahimiza wachezaji.
B. Kocha alikuwa hawapongezi bila kuwahimiza wachezaji.
C. Kocha alikuwa hawapongezi ila kuwahimiza wachezaji.
D. Kocha hakuwa akiwapongeza wala kuwahimiza wachezaji.

**21.** Maneno yaliyopigiwa mstari ni
Vijana <u>hawa</u> walifika <u>mapema</u> <u>lakini</u> <u>wale</u> walichelewa.
A. nomino, kielezi, kiunganishi, kiwakilishi
B. kivumishi, kielezi, kiunganishi, kiwakilishi
C. kiwakilishi, kivumishi, kielezi, kivumishi
D. kivumishi, kiwakilishi, kiunganishi, kivumishi

**22.** Chagua jibu lenye maneno **yasiyoambatanishwa** ipasavyo.
A. kikuku - mguu
B. kipini - pua
C. ushanga - shingo
D. kikuba - kiwiko

**23.** Ni jibu lipi lenye nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi?
A. nyweka - nywesha
B. ogopa - ogofya
C. saka - usasi
D. amini - aminifu

**24.** Onyesha sentensi iliyo katika hali ya mazoea.
A. Magari ya usafiri wa umma hayapiti hapa.
B. Mvua ya masika haijaanza kunyesha.
C. Mto ukifurika hawatavuka.
D. Vazi hilo halikushonwa vizuri.

**25.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
Baharia huyu amevaa koti zuri.
A. Baharia hawa wamevaa makoti mazuri.
B. Mabaharia hawa wamevaa koti zuri.
C. Mabaharia hawa wamevaa makoti mazuri.
D. Baharia hawa wamevaa makoti mazuri.

**26.** Sogora kwa ngoma ni kama _____ kwa mapambo
A. mhunzi
B. kaimu
C. mjumu
D. sonara

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**27.** Ukubwa wa sentensi:

Mtoto huyu hataweza kukibeba kikapu hicho ni

A. Toto hilo halitaweza kulibeba kapu hili.
B. Jitoto hili halitaweza kulibeba kikapu hicho.
C. Toto hili halitaweza kulibeba kapu hilo.
D. Kitoto hiki hakítaweza kulibeba kapu hilo.

**28.** Ni jibu lipi lenye maneno ya aina moja?

A. ua, embe, chelewa
B. andikiwa, ruka, chezesha
C. dawati, agiza, kaka
D. waka, salama, tena

**29.** Neno **mkadamu** lina silabi ngapi?

A. 4
B. 3
C. 7
D. 6

**30.** Teka alikabiliwa na shida nyingi maishani. Akajitahidi kuzisuluhisha na hatimaye hali yake ikaimarika. Methali inayojumuisha ujumbe huu ni

A. Mbio za sakafuni huishia ukingoni.
B. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
C. Mtembezi hula miguu yake.
D. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40**

Amani ni hali ya utulivu ambayo hupatikana pasipo na vita wala machafuko yoyote. Mara nyingi hali hii hupatikana pasipo na gharama yoyote. Hili hasa ndilo linalowafanya wengi kutotilia maanani umuhimu wa amani. Lakini kama walivyosema wahenga, asiyejua thamani ya mwangaza aingie gizani. Ushahidi kuhusu matokeo ya ukosefu wa amani umeenea vururu katika jambu nyingi.

Yamkini nikikuuliza kama unajua umuhimu wa amani utakuwa mwepesi wa kusema ndio. Lakini pengine ukituama na kuwazia matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea karibu nawe, au hata kwa mchango wako binafsi, utagundua kuwa umewahi kuchangia kuvuruga amani kwa njia moja au nyingine. Unakumbuka siku ambapo ulieneza uvumi kuhusu mwenzako darasani? Labda ulilichukulia tukio hilo kuwa la kawaida tu. Ambalo hukujua ni kwamba kwa kufanya hayo, ulimsababishia kutengwa na marafiki, ukamfanya ajione duni na kumnyima amani. Bila shaka, ulimwumiza sana kihisia. Ieleweke kuwa tabia ni ngozi. Matendo ya aina hii yasipothibitiwa huweza kuwa msingi wa kusambaratisha mshikamano wa kitaifa baadaye.

Watu wengi **huinyoshea serikali kidole** wakati yanapozuka machafuko yoyote nchini. Utawala uliopo hukashifiwa kwa kushindwa kutekeleza jukumu lake la kulinda raia wote. Hata hivyo watu wawa hawa ndio kwa mfano wanaowasetiri washukiwa serikali inapojaribu kunyoosha mkono kuwafikia. Watu hawa wakiombwa na vyombo vya dola watoe ushahidi utakaochangia kushtakiwa kwa washukiwa wenyewe, wao hufyata ndimi zao. Isitoshe, wanasiasa wachochezi hukimbilia kutafuta hifadhi za makabila yao pale wanapokabiliwa na mashtaka ya kuvuruga amani nchini. Hata pale tunapodekeza hali hii, ni vyema tukumbuke kuwa vita havina macho.

Gharama ya kutokuwepo amani huwa kubwa katika jamii yoyote ile. Watu hulemazwa huku wengine wakipoteza roho zao. Mali yaliyochumwa kwa muda mrefu huharibiwa katika muda wa kufumba na kufumbua. Katika maeneo kama haya, wawekezaji hutoweka, jambo ambalo huwanyima vijana nafasi za kujiendeleza. Maeneo kama haya huselelea nyuma kiuchumi.

Ni vyema tumaizi kuwa jukumu la kulinda amani haliwezi kuachiwa asasi za kiusalama pekee. Lazima tushikane mikono kupigana na hali yoyote inayotishia usalama wetu kwa hali na mali. Taasisi za kielimu na kidini ziwe katika mstari wa mbele kuhubiri amani. Wanaotumia madhabahu kuwagawanya watu kwa misingi ya kidini watengwe na kukashifiwa. Viongozi wa kijamii nao wachangie kupiga vita mila potovu kama vile wizi wa mifugo na uvamizi. Wanasiasa wachochezi watemwe wakati wa uchaguzi. Vijana nao wajiunge katika vilabu vya kutangaza amani kote nchini.

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**31.** Chagua jibu sahihi kulingana na aya ya kwanza.

A. Amani ni hali ya utulivu palipo na vita.
B. Watu wengine hupuuza thamani ya amani.
C. Ukiingia gizani utajua umuhimu wa amani.
D. Gharama ya amani huwa kubwa sana.

**32.** Ni kweli kusema kuwa,

A. lazima msomaji anajua umuhimu wa amani.
B. Visa vya utovu wa amani hutokea karibu na watu.
C. Amani yetu huvurugwa na wale tunaowazia.
D. Amani huweza hata kuvurugwa na matendo tusiyotilia maanani.

**33.** Unapoeneza uvumi dhidi ya mtu fulani,

A. humwumiza kihisia na kumfanya akose kujistahi.
B. unawatenga marafiki zako na kujiumiza kihisia.
C. unamkosesha utulivu na kumwinulia hadhi yake.
D. huwezi kujua kuwa ufanyayo si haki.

**34.** Msimamo wa mwandishi ni kuwa

A. vurugu za watoto ndizo zinazosambaratisha jamii.
B. ukosefu wa amani humfanya mtu ajiondoe katika jamii.
C. tabia isipodhibitiwa mapema inaweza kuleta utengano katika jamii.
D. mambo madogomadogo hayawezi kuathiri misingi ya kijamii.

**35.** Ni kawaida ya watu

A. kukashifu watawala utulivu unapokosekana.
B. kuwakashifu wahasiriwa usalama unapodorora.
C. kuitetea serikali usalama unapovurugika.
D. kujua umuhimu wa amani pale inapokosekana.

**36.** Raia katika kifungu wamelaumiwa kwa

A. kutowajua wanaotekeleza vitendo vya kihalifu.
B. kuwaonya wenzao wanapotaka kutoa ushahidi.
C. kuwafichua washukiwa wanaotafutwa na serikali.
D. kukosa kusaidia serikali kuwahakikishia usalama.

**37.** Njia bora **zaidi** ya kukabiliana na wanasiasa wanaoeneza chuki katika jamii ni

A. kueneza habari zao katika vyombo vya habari.
B. kuwaondoa mamlakani wakati wa kupiga kura.
C. kuwatia mbaroni na kuwanyamazisha kabisa.
D. kuwaacha wapige domo kwani watanyamaza tu.

**38.** Yafuatayo ni madhara ya ukosefu wa amani **isipokuwa**,

A. watu kupoteza maisha.
B. uharibifu wa mali.
C. kudidimia kwa uchumi.
D. kuenea kwa ukame.

**39.** Wazo kuu linalojitokeza katika aya ya **mwisho** ni kuwa

A. mila potovu ndizo zinazovuruga amani nchini.
B. asasi za kijamii hazihusiki katika kudumisha amani.
C. jukumu la kulinda amani ni la kila mwanajamii.
D. tukishirikiana katika vita amani ya kudumu itapatikana.

**40.** **Huinyoshea serikali kidole** ni sawa na

A. kuilaumu serikali.
B. kuikejeli serikali.
C. kuikosea serikali.
D. kuitukana serikali.

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali kuanzia* **41** *mpaka* **50**

Nilipomaliza mtihani wa kitaifa wa darasa la nane, nilijua kuwa ningepata liziko ndefu kuliko kawaida. Baada ya kukaa mjini kwa siku mbili-tatu, niliwaomba wavyele wangu kibali cha kuenda kijijini kuwazuru babu na bibi. Japo sikuzielewa sana shughuli za shamba, nilijua kuwa msaada wowote kwa wazee wale ungewafaa sana hasa ikizingatia kuwa walikuwa **wamebugia chumvi ya kutosha**. Waama, auni ni auni hakuna auni duni.

Siku ya safari ilipowadia, baba na mama walinipeleka kituoni pa mabasi na kuniaga. Nilijawa na wahaka kiasi na kujiuliza, "Itakuwaje gari likinipitisha? Je, nitaweza kukitambua kituo chao vizuri?" Nilitoa shajara yangu na kuhakiki tena maelezo niliyoandika. 'Njia panda baada ya stoo mbili, nishike njia ya kulia'. Hata nilimwuliza utingo kama alikifahamu kituo hicho naye akanihakikishia nisiwe na shaka. Nilimshukuru na kutulia.

Safari yangu ilikuwa shwari bila shari. Njiani nilijisaili maswali anuwai. Nilijiona nikawafaa babu na bibi kwa njia nyingi. Nikajionea nikiwafunza vijana wa mashambani mambo mengi ya mji. "Nitawatoa ushamba kabisa," nikajiambia. Kutahamaki, gari lilisimama, utingo akaniashiria nishuke na kumsaidia kutua mzigo wangu. Kinyume na matarajio yangu, babu alikuwa pale kituoni akinisubiri. Nilimlipa hamali anibebee furushi lile la bidhaa, nikajibebea shanta yenye nguo zangu na kumwandama babu unyounyo.

Kijiji cha akina babu kilijaa utulivu wa kuridhisha. Nilipokelewa vizuri. Hata hivyo, jambo moja lilinisumbua akilini. Vijana wenzangu walinisalimia kwa heshima lakini hakuna aliyesema jingine zaidi ya salamu. Sijui kama ni mimi niliyefikiria hivyo, lakini nilihisi kiasi fulani cha chuki hasa kutoka kwa wazazi wa kike. Jambo hili lilininyima raha kwani nilidhani kijijini kulitawaliwa na hisia za udugu kama nilivyozoea kusikia ikiwa haya yalifanyika mjini ningeelewa.

Siku moja, mkazahau aliniita chemba na kunipasulia mbarika. Mavazi yangu hasa ya suruali zilizonibana ndiyo yaliyowafanya wengi kujitenga nami. Kumbe kile nilichoita ustaarabu kutokana mjini kilionekana kama utovu wa maadili mjini. Hapo ndipo nilipoujua ukweli ya methali, **ukila pamwe na namiri, igiza zao desturi**. Mkazahau alinifunza mengi kuhusu maisha ya mashambani. Nami nikaafiki methali kuwa kinolewacho hupata.

Polepole, nilianza kuwapata wenza. Tulifanya mengi pamoja. Tulibeba maji kwa mitungi migongoni na kuleta matita ya kuni msituni. Nilizifurahia shughuli hizi sana. Kila mara wenzangu hawakusita kunitahadharisha, "Usiuguse upupu huo utawashwa" au "chaka hilo linaweza kuwa na nyoka tahadhari!" Hata wakati wa kurudi mjini ulipofika, niliona uchungu kutengana na wasena wale.

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

41. Ni maelezo yapi yaliyo sahihi?
   A. Ilikuwa likizo ya mwisho katika darasa la nane.
   B. Msimulizi alisafiri pindi tu alipofunga shule.
   C. Mwandishi hakupendelea kuishi mashambani.
   D. Mwandishi alinuia kuwasaidia babu na nyanya yake.

42. Msemaji anakiri kwamba,
   A. hakuzoea kushiriki shughuli za shambani.
   B. ilikuwa mara ya kwanza kumzuru bibi yake.
   C. anazifurahia sana kazi za mashambani.
   D. hatajifunza shughuli za shambani.

43. Maneno **wamebugia chumvu ya kutosha** yametumia tamathali gani ya usemi?
   A. sitiari
   B. nahau
   C. chuku
   D. tashhisi

44. Kulingana na aya ya pili, tunaweza kusema kwamba mwandishi,
   A. ni mwenye papara
   B. hana mwao kuhusu aendako
   C. ni mwoga
   D. ni mwenye makini

45. Utoaji bora wa huduma unaojitokeza kwa kuwa,
   A. babu alimlaki msimulizi kituoni.
   B. hamali alimbebea mwandishi furushi lake.
   C. utingo alimpa mwandishi msaada aliohitaji.
   D. mwandishi aliandika maelezo kwenye shajara.

46. **SI** kweli kusema kuwa,
   A. mwandishi alibebewa mizigo yake yote.
   B. msimulizi hakutaabika kufika kwa babu.
   C. mwandishi hakutarajiwa kupokelewa kituoni.
   D. msimulizi alitarajia kuwafunza wenyeji wale ustaarabu.

47. Jambo lililomsumbua mwandishi ni
   A. kukosa kusalimiwa na wanakijiji.
   B. kutengwa na baadhi ya wanakijiji.
   C. kutowaona vijana kijijini.
   D. hali ya utulivu iliyoshamiri kijijini.

48. Wazazi wa kike walimwonyesha chuki msimulizi kwa kuwa
   A. hakupenda kuvalia jinsi alivyoagizwa.
   B. aliwapotosha wanao kwa mienendo ya mjini.
   C. alipenda kuwadharau wanakijiji.
   D. alikiuka utamaduni wao

49. Methali **ukila pamwe na namiri, igiza zao desturi** inahimiza
   A. tukiingiliana na watu wenye sifa kama zetu tujaribu kuwa tofauti.
   B. tukijua kuwa watu wana sifa tofauti tujiepushe tusiathiriwe na nyendo zao.
   C. tukiingiliana na watu wenye sifa tofauti tutafute mbinu za kuingiliana vizuri nao.
   D. Tukiwa na sifa tofauti tuwahimize wengine wajaribu kuwa kama sisi.

50. Aya ya mwisho inatufunza kuwa,
   A. kugusa upupu humfanya mtu awatambue marafiki.
   B. uhusiano unaweza kuimarishwa hata katika mazingira mapya.
   C. kukemewa kwa sauti humfanya mtu atambue mazingira.
   D. Uchungu wa kutengana huzidi mtu anapoenda mjini.

**JESMA K.C.P.E PREDICTION WILL BE OUT ON 8TH MARCH 2021**
**DONT MISS!!!**

Ecolebooks.com

Scanned with CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM